


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Simu+25526 2782443
Barua pepe: acl.njombe@lands.go.tz
Tovuti: www.lands.go.tz



Ofisi ya Ardhi Mkoa,
S. L. P. 776,
NJOMBE.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. LD/NJB/8630/13

19 Septemba, 2024

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania,
S.L.P. 938,
DAR ES SALAAM.

YAH: KIWANJA Na. 6 KITALU 'C' KILICHOPO ENEO LA IKELU
MAKAMBAKO MJINI

Tafadhali husika na somo hapo juu.

2. Halmashauri ya Mji Makambako walipokea maombi ya umilikishwaji wa kiwanja tajwa kwa Kampuni ya FUJIAN HEXINGWANG INDUSTRY TANZANIA CO. LIMITED. Nyaraka zilizoambatishwa na maombi hayo zinaonesha kuwa Waombaji walipata ardhi husika kutoka kwa Wakazi wa asili wa eneo hili baada ya kulipa fidia ya ardhi hiyo na maendelezo kupitia utaratibu wa fidia ulioaratibiwa na Halmashauri ya Mji Makambako.
3. Matumizi ya kiwanja hiki ni Kituo cha kupoozea umeme ambao utatumika kwa ajili ya kuhudumia kiwanda kinachotarajiwa kujendwa katika kiwanja namba 4 Kitalu C Ikelu ambacho Kampuni ya FUJIAN HEXINGWANG INDUSTRY TANZANIA CO. LIMITED inafanya uwekezaji baada ya kumilikishwa kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania TIC).
4. Kampuni ya FUJIAN HEXINGWANG INDUSTRY TANZANIA CO. LIMITED imesajiliwa nchini chini ya Sheria ya Makampuni Na. 12 ya mwaka 2002 na Wanahisa wake wote ni raia wa Nchi ya China na hivyo kuwa ni Kampuni ya kigeni.
5. Kutokana na Kampuni hii kuwa ni ya kigeni, na kwa mujibu wa Fungu la 19 la Sheria ya Ardhi na. 4 ya Mwaka 1999, umilikishaji kwa Kampuni hii unatakiwa kufanywa kwa ajili ya uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Hivyo, Ofisi imetayarisha

Fomu ya Ardhi namba 1 (Designation of land for Investment Purposes) kwa ajili ya kuitangaza ardhi hii kuwa ya uwekezaji ili taratibu nyingine ziweze kuendelea,

6. Pamoja na barua hii naambaisha nyaraka zifuatazo kwa ajili ya kukamilisha taratibu zinazohusika:

- i. Mchoro wa Mipangomiji
- ii. Ramani ya Upimaji
- iii. Hati ya kuandikishwa Kampuni ya FUJIAN
- iv. Memorandum and Articles of Association
- v. Vivuli vya passport za Wanahisa
- vi. Certificate of Incentives
- vii. Barua ya historia kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako na
- viii. Land Form No. 1

Naomba kuwasilisha.



B.T. NSAJI

**KAIMU KAMISHNA WA ARDHI MSAIDIZI
MKOA WA NJOMBE**

NAKALA:

Katibu Tawala (M)
S.L.P. 668,
NJOMBE.

Kamishna wa Ardhi,
S.L.P. 2908,
DODOMA.

Mkurugenzi wa Mji,
Halmashauri ya Mji, Makambako,
S.L.P. 405,
MAKAMBAKO.

Fujian Hexingwang Industry Tanzania CO. Limited,
S.L.P. 63069,
MKURANGA-PWANI.